HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI DR. CHEGENI,

S.L.P 66,

BUSEGA-SIMIYU

TAREHE……..

KUMB. Na……

Mwanafunzi ……

S.L.P ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DR. CHEGENI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Dr.Chegeni ni ya kutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (Wavulana na Wasichana). Ipo umbali wa 1.1km kutoka standi ya magari iliyopo Nyashimo (Nyashimo Centre) magharibi mwa barabara kuu ya sirali-mwanza.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/202 ndani ya siku 14.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare ya shule:

i. Sare ya shule ni suruali yenye marinda na pindo la chini (Mguu wa suruali), rangi ya kitambaa ni “Dark Grey” 2 kwa wavulana na Sketi Dark Grey 2 kwa wasichana. Aina yakitambaa kimeambitanishwa kwenye form yakujiunga na Shule. Viatu vyeusi visivyo na Kamba (Simple), Soksi Nyeusi kwa Wavulana na Nyeupe kwa Wasichana.

ii. T-shirt ya rangi Grey (Kijivu) zinapatikana kwa Mzabuni (Nyashimo) kwa Wavulana na Wasichana

iii. Tai yenye rangi ya damu ya mzee yenye michirizi ya kijivu (Grey) zinapatikana pia kwa mzabuni Nyashimo kwa wavulana na wasichana.

iv. Sweta la rangi ya damu ya mzee.

v. Nembo ya shule inayopatikana kwa Mzabuni pia.

vi. Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi upande wa kushoto wa bega kuwe na namba ya kidato husika (I, II, III au IV) kwa kitambaa cha rangi ya sketi ya kwa wasichana na suruali kwa wavulana.

vii. Sare za michezo kwa shule hii ni:-

- T –shirt za rangi nyekundi na michirizi meupe kwa Wavulana na Wasichana
- Bukta za rangi nyekundu zenye michirizi meupe ubavuni kwa Wavulana na Wasichana
- Raba nyeupe kwa wasichana na Njumu za mpira (Raba zenye meno kwenye soli) kwa Wavulana
- Soksi rangi Nyeusi zenye michirizi meupe kwa juu kwa Wavulana na wasichana

2.2 Vifaa vya kujifunzia: Daftari kubwa 10 (counter books), Kalamu za wino na penseli, Rula, Mkebe wa hesabu (Mathematical set).

2.3 Ndoo kubwa ya maji pamoja na Ufagio wa nje (Chelewa). (KWA WASICHANA)

2.4 Reki na Jembe (KWA WAVULANA)

NB: KWA VIFAA NAMBA 2.3, WANAOTAKIWA KUJA NAVYO NI WANAFUNZI WAKIKE TU. KWA VIFAA NAMBA 2.4 WANAOTAKIWA KUJA NAVYO NI WANAFUNZI WAKIUME TU.

2.5 Mchango (TSH.5000 KWA MWAKA MZIMA 2021) KWA AJILI YAKULIPIA BIMA YA AFYA **(CHF)** kwa wasio na BIMA YA AFYA. **NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE WA DR. CHEGENI SEKONDARI KUKATIWA BIMA YA AFYA KAMA HANA.**

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. **Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.**

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

a) **Mahudhurio** mazuri kila shughuli ndani ya nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
b) Kushiriki kwa makini **kujifunza kwa bidii** shuleni na nyumbani.
c) **Kuwahi** katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) **Kutunza usafi** wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
f) **Kuvaa sare ya shule wakati wote** unapotakiwa.
g) **Kuzingatia ratiba ya shule** wakati wote.
h) Kutunza mali za umma.

1.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

vii. Kudharau Bendera ya Taifa.

viii. Kuwa mjamzito/kupata mimba.

ix. Kuoa au kuolewa.

x. Kutoa mimba.

xi. Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

xiii. Kuwa na simu ya mkononi.

1.0 MAMBOMENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) **Medical Examination form** ambayo itajazwa na mganga mkuu wa wilaya ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule **mara utakaporipoti shuleni**. KIAMBATISHO “B”

b) **Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba** wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi/ mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. KIAMBATISHO” A”

c) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

JAPHET SIRIKWA JOSEPH

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI DR. CHEGENI.

KIAMBATISHO B:
GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS
DR. CHEGENI SECONDARY SCHOOL

PART A:

Full name ……..……

Age: ……height (cm) ……. sex……. weight……

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for joining secondary school. The examination should include the following categories (I –III) each category or Sub category of which, will render the applicant ineligible in each of a defect. Pregnancy (Plano test), category IV will render a girl student ineligible.

I.

(a) Eye – sight …….

(b) Hearing ……...

(c) Speech ……

(d) Venereal disease (HIV) ……...

(e) Leprosy and T.B Disease ……

(f) Epilepsy ……...

(g) Spleen …….

(h) Chest/Abdomen …….

(i) Blood Coat ……. (Red and White)

(j) Urinalysis ……...

II. Neuroses ……

III. Additional information e.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family/heritable disease (e.g. sickle cell) inability to eat certain food etc.

……

……

IV. Pregnancy ……

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named school child and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit time secondary Education course.

Name and signature ……...

Designation ……

Station ……

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

i. Mahuzurio mazuri kila shughuli ndani ya nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
ii. Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
viii. Kutunza mali za umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
viii. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kutoa mimba.
xi. Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xiii. Kuwa na simu ya mkononi.